**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

Mwenyekiti wa taifa wa CHADEMA  Mheshimiwa Freeman Mbowe

Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chadema Dr. Wilbrod Slaa

Viogozi wakuu wa CHADEMA

Mabibi na Mbwana

Ni faraja na heshima kubwa kwangu kukaribishwa kuja kutoa mada leo katika kikao hiki cha Chama Kikuu cha Upinzani nchini Tanzania

Mwaliko wenu kwangu ni ishara ya mahusiano yanyozidi kukua na kuboreka kila siku kati ya chama cha siasa cha CHADEMA na sekta binafsi ya Tanzania. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya viongozi wenzanguu wa sekta binafsi nchini, natoa shukurani zangu na kuomba uhusiano wetu uendelee kuboreka.

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

Ahsante sana.

Katika kutayarisha mada yangu, nimetafakari sana nianzie wapi.

Nikaona ni bora nianzie katika swala zima la mahusiano kati ya sekta binafsi nchini na vyama vya siasa kwa ujumla nikielekeza mawazo yangu zaidi kwa CHADEMA.

Nimeamua kuzungumizia utata uliopo katika kutofautisha sera za uchumi za chama tawala na vyama vya upinzani hususan CHADEMA hasa kwa mtazamo wangu mimi kama mdau wa sekta binafsi na mdau mzawa.

Katika utafiti wa haraka niliofanya, mimi nimeona kwamba inawezekana tatizo lililopo linatokana na tofauti zilizopo kati ya matamshi ya itikadi ya chama husika kama ilivyoainishwa kimaandishi ya katiba yake au party manifesto na imani halisi za viongozi wa chama ambazo mimi naamini ndizo

zinazoamua mwelekeo wa matendo yao binafsi.

Lakini labda kabla sijajikita sana katika kuzungumzia itikadi na matendo, nitoe mfano ambao natumaini utasaidia kuonyesha umuhimu wa itikadi katika kukiwezesha chama siyo tu kuwa na ushawishi katika jamii, bali pia kuwa na vigezo vya utendaji na uwajibikaji ambavyo vitakiwezesha chama kudumisha uhai wake kisiasa.

## Makosa Makuu Matatu Ya Kiitikadi Yaliyoathiri Mfumo na Uimara wa Uchumi wa Tanzania Tangu Uhuru

Nionavyo mimi, uchumi wa nchi yetu umekuwa ukiyumba tangu tulipopata uhuru zaidi ya nusu karne iliyopita kwa sababu ya kutokuwepo msimamo madhubuti wa kiitikadi katika siasa zetu na usimamizi wa uchumi kwa ujumla.

Kuyumba huku kwa uchumi kumetokana na makosa makuu matatu ya kimkakati yaliyofanywa na mlolongo wa watawala wa nchi hii tangu siku za mwanzo za uhuru mpaka leo.

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

## Kosa la kwanza: Tulijiandaa Kupata Uhuru wa Bendera Siyo wa Kiuchumi

Mwaka 1961 wakati Tanganyika ikipata uhuru, watawala wetu walifanya maadalizi ya kupokea mamlaka za kuendesha serikali kisiasa na kiutawala lakini hakuna ushahidi kwamba kulikuwa na mkakati maalum wa serikali kushika hatamu za uchumi aidha moja kwa moja au kupitia wananchi wake.

Pia kulikuwa hakuna muafaka wa kitaifa kuhusu dhana ya uzawa. Watawala waliamua kwamba watu wote waliokuwa wakiishi Tanganyika chini ya utawala wa Malkia wa Uingereza wakati wa uhuru watakuwa raia wa Tanzania. Hapakuwekwa bayana tofauti kati ya uraia na uzalendo au uzawa.

Kosa lililofanyika hapa ni kwamba kwa kutotofautisha kati ya raia wazawa na raia wengine, serikali ilifuta kimaandishi tu tofauti za uwezo wa kushiriki katika uchumi zilizokuwepo katika jamii yetu baada ya karne nyingi za kutawaliwa na mataifa ya kigeni ambapo raia wazawa walizuiwa kisheria

kumiliki biashara kubwa na uchumi wa nchi uliendeshwa kwa kiasi kikubwa sana na raia walioletwa nchini na serikali ya kikoloni.

Hivyo basi, baada ya kupata uhuru mwaka 1961, serikali mpya ya wazawa ilisimamia utawala, ulinzi na usalama na mambo mengine yahusuyo dola lakini usimamizi na uendeshaji wa mambo ya biashara na uchumi vilibaki mikononi mwa watu hao. Iliichukua serikali ya awamu ya kwanza miaka sita kabla haijagundua kosa ililofanya.

## Kosa la Pili: Azimio la Arusha Lilibomoa Badala ya Kujenga

Mwanzoni mwa mwaka 1967, serikali kupitia chama tawala wakati ule cha TANU ilitangaza mabadiliko makubwa ya kisiasa nchini. Kwa mara ya kwanza chama kilitangaza falsafa yake ya ujenzi wa jamii bora na uendeshaji wa kiuchumi na kuiita Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo inaweza kuitwa pia siasa ya mrengo wa kushoto.

Hii ilikuwa ni baada ya serikali kubaini kwamba mkakati wake wa kusimamia uchumi ulikuwa

hauleti tija iliyotegemewa. Kuliibuka katika majukwaa ya kisiasa dhana ya wanyonge na mabepari au makabaila, dhana ya wanyonyaji na wanyonywaji. Bila shaka wanyonge walikuwa ni raia wazalendo na wanyonyaji walikuwa ni wadau wa sekta binafsi ya wakati ule ambayo ilirithi hatamu za kuendesha uchumi kutoka kwa wakoloni.

Baada ya miaka mitatu (mwaka 1970), serikali ilitangaza na baadaye kutekeleza nia yake ya kutaifisha mali za watu binafsi ambao iliwatuhumu kuhodhi uchumi wa nchi na kunyonya raia wazawa wanyonge.

Tatizo kubwa la sera hii ni kwamba badala ya serikali kuhamisha uwezo wa kibiashara na kuendesha uchumi kutoka kwa hao raia wa nje au wa kuja na kuupeleka kwa raia wazawa, ilitangaza vita kwa sekta binafsi kwa ujumla wake bila kutofautisha washiriki. Ilipigilia msumari jeneza la uchumi huria kwa kutangaza kwamba Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi tu. Pia ilifanya kampeni ya nguvu ya kisiasa iliyolenga kujenga chuki kati ya raia wa kawaida na sekta binafsi. Serikali ilikamata hatamu za uchumi zote, ikaanziasha mashirika ya umma yaliyofanya

biashara za kila aina kuanzia ndogo kama vile kuuza kanga za kina mama na sukari mpaka kubwa zilizoshiriki katika uzalishaji wa vipuri vya viwanda na mashine.

Jambo la kushangaza ni kwamba japokuwa Watanzania wazawa walikatishwa tamaa kabisa au kutishwa wasifanye biashara, raia wenzao wa kigeni au wazalendo wa kuja waliendela na biashara kidogo ambazo serikali haikuzidhibiti na baada ya muda si mrefu walirejea kuwa na ushawishi mkubwa katika uendeshaji wa uchumi wa nchi yetu.

Sera za Ujamaa na Kujitegemea hazikudumu kwa muda mrefu kwani ziliharibu uchumi na kufanya maisha ya watu nchini kuwa magumu sana. Mashirika karibu yote yaliyoanzishwa na serikali yalifilisika kutokana na uendeshwaji mbaya na sera mbaya za uchumi zilizotawaliwa na serikali kuingilia mwenendo wa masoko kama vile kuamuru bei za bidhaa madukani na udhibiti wa fedha za kigeni

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

Miaka ya 1981-82 Watanzania walishuhudia serikali ikiadhibu raia kwa makosa yake yenyewe pale ilipotangaza vita dhidi ya " wahujumu " wa uchumi wakati mhujumu mkuu alikuwa ni sera mbovu za uchumi ambazo chama tawala kiliziweka kwa miaka ishirini tangu uhuru. Vita hii iliwakumba watu wote lakini walioathirika zaidi ni raia wazawa ambao walikuwa wameanza kujaribu kujenga uwezo wa kufanya biashara. Wengi walinyang'anywa mali zao na hata kufungwa jela bila sababu za msingi. Wazazi wangu mimi ni pamoja na wahanga wa sera hizi za miaka ya Uhujumu wa Uchumi.

Wakati wote huu serikali ilikuwa ikijaribu bila mafanikio na kwa gharama kubwa kuonyesha kwamba itikadi yake ya Ujamaa ni bora kuliko zile zilizoruhusu uchumi huria na ushiriki wa sekta binafsi katika nyanja zote muhimu za uchumi. Hili lilikuwa ni kosa kubwa la kimkakati lililofanywa na serikali yetu na kuiathiri sana sekta binafsi ya nchi yetu, hasa sekta binafsi ya Watanzania wazawa.

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

## Kosa la Tatu: Sera Za Ubinafsishaji za Miaka ya Tisini Zilihamisha Hatamu za Uchumi Kutoka Seriakalini na Kurudi Kwa Wale Waliorithi Uchumi Kutoka Kwa Mkoloni

Baada ya serikali kubani makosa yake katika miaka ya mwisho ya serikali ya Awamu ya Kwanza, ilifanya maamuzi magumu ya kuachana na sera za uchumi za mrengo wa kushoto na kuanza kuleta mabadiliko yaliyoendana na mtazamo wa uchumi huria na serikali ikajiondoa kwenye biashara lakini ilifanya hivyo bila kuzingatia umuhimu wa ushiriki wa Watanzania wazawa katika uchumi huo mpya.

Makampuni yaliyobinafsishwa hasa yale nyeti kama vile mabenki, kampuni ya simu, migodi ya madini, mashamba makubwa, n.k. yalinunuliwa na watu walewale walionyang'anywa miaka ya sabini. Mengine yaliachwa yakafa bila sababu za msingi na kusababisha hasara.

Badala ya kutumia nafasi ya kipekee iliyokuwa nayo kukabidhi mashirika hayo kwa watanzania wazawa ili wayatumie kujenga msingi wa ushiriki wao katika uchumi, serikali iliwapa watu wa nje

au kama ilishindikana iliyaacha yafe.

Leo, zaidi ya miaka hamsini tangu nchi yetu ipate uhuru, mwananchi mzawa anendelea kuwa mdau dhaifu katika uchumi wake na ushiriki wake unaendelea kubezwa na kudhoofishwa na sera zenye malengo yasiyoeleweka. Kwa kiasi kikubwa mimi nalaumu sera za uchumi zinazotokana na itikadi ya siasa na uchumi ambayo haikuwahi hata siku moja kulenga kumuweka mwananchi Mtanzania katika nafasi ya kudhibiti na kuendesha uchumi wa nchi yake kama zifanyavyo nchi nyingine duniani. Hili ni kosa la tatu lililofanywa na watawala wetu.

Nimesema yote hayo kwani nataka kuunganisha kimantiki tatizo la maelewano kati ya sekta binafsi ya Tanzania leo na vyama mbali mbali vya siasa nchini.

Tuanze na itikadi ya CHADEMA. Nimenukuu vipengele vichache vya itikadi ya CHADEMA vinavyohusu mambo ya uchumi kutoka kwenye tovuti yenu.

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

*3.B. Itikadi ya CHADEMA*[1]

*3.1.1 CHADEMA ni chama cha itikadi ya MRENGO WA KATI (center party).*

*3.1.2 CHADEMA ni chama kinachoamini kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi kwa kutumia raslimali za nchi yetu bila kuathiri uhuru wa Taifa, na kuhakikisha kuwa umma kwa ujumla unanufaika na raslimali zao.*

*3.1.3 CHADEMA inaamini katika kujenga na kuimarisha uchumi wa soko huru, utakaoheshimu na kulinda haki na mali za watu, biashara huru na sekta ya watu binafsi bila kupoka mamlaka ya umma katika maeneo nyeti hususani pale penye hitilafu ya soko au penye maeneo nyeti ya kiuchumi. Tunaamini katika soko huru sio soko holela.*

1. Source: CHADEMA Website – Jan 2014

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

*3.1.7 CHADEMA inaamini katika siasa ambazo ziko juu ya vyama zenye kusimamia zaidi maslahi ya Taifa.*

*3.1.11 CHADEMA inaamini katika kujenga uwezo wa wazawa katika kumiliki na kuendesha uchumi.*

| Issue | Isemavyo Itikadi ya CHADEMA | Tatizo |
|---|---|---|
| Mrengo wa Itikadi ya Chama | 3.1.1 CHADEMA ni chama cha itikadi ya MRENGO WA KATI (center party). | Watanzania walio wengi wakiwemo wasomi hawajui tofauti kati ya mirengo mbalimbali ya itikadi za kisiasa kwani jamii yetu haina historia ya migongano ya kiitikadi kama ilivyo hasa katika nchi za Ulaya. Kwa sababu hiyo kusema kwamba CHADEMA kinafuata siasa zenye mrengo wa kati hakuielezi chochote jamii |

kwa kiasi cha kutosha kuwawezesha kukitofautisha na vyama vingine.

Chama pekee ambacho kila Mtanzania anakifahamu kama chama tawala kwa sasa hivi kiko kwenye harakati ya kubadilisha mrengo wa itikadi yake tangu miaka ya tisini. Ni mategemeo yangu kwamba muda muafaka ukifika kitatangaza kwamba kinafuata siasa za mrengo wa kati kama CHADEMA. Katika mashindano ya ushawishi wa umma kuhusu itikadi, CCM itaizidi nguvu CHADEMA hasa kwa vile itakumbusha wananchi kwamba ina uzoefu wa kutawala wakati CHADEMA itataka kufanya majaribio

Tunaamini katika soko huru sio soko holela.

Kuwepo kwa sentensi hii katika ibara ya 3.1.3 kunaashiria kuwepo kwa mashaka katika fikra za Wana-CHADEMA kuhusu ubora wa uchumi huria

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

kwani hakuna mfano wa nchi inayojulikana duniani kwa kuwa na uchumi holela. Hayo ni maneno ya kubeza uchumi huria yatumiwayo na wahafidhina wa siasa za mrengo wa kushoto.

Jamii inahitaji ujumbe usiokuwa na walakini au mashaka yoyote kuhusu msimamo wa kiuchumi wa chama cha siasa

Tofauti kati ya itikadi na vitendo vya chama na viongozi wake

CHADEMA inaamini katika kujenga uwezo wa wazawa katika kumiliki na kuendesha uchumi.

Hatujaona tofauti ya kiitikadi kati ya CHADEMA na vyama vingine vya siasa katika utekelezaji wa sera za uchumi. Vyama vyote vikiwemo na NCCR-Mageuzi, CUF na vinginevyo ni populist, anti-private sector katika matamshi na vitendo.

Mifano tumeiona kwenye sekta ya madini makampuni yalivyoshambuliwa na vyama vyote vya upinzani hasa

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

CHADEMA kwa makosa ambayo kama yalikuwepo yalikuwa si ya mfumo wa uchumi bali udhaifu wa kiutendaji serikalini na labda rushwa. Badala ya kuwaadabisha watendji, vyama vya upinzani vilielekeza hasira zao kwa wawekezaji ambao kwa mtazamo wangu hawakuwa na hatia. Kitendo hiki kilifanya sekta binafsi itilie mashaka msimamo wa CHADEMA kuhusu uwekezaji nchini.

Seriakali iliyopo madarakani imerudisha sera za serikali kushika hatamu za uchumi (Commanding Heights) kinyemela, imeanzisha mashirika mengi ya umma yasiyo na mipangilio ya kibajeti au uwajibikaji kiutendaji mambo ambayo ni kinyume na itikadi za CHADEMA lakini lakini CHADEMA haijachukua hatua zozote dhidi ya mwenendo huu unaorudisha nchi

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

nyuma kiuchumi
Tanzania inatumia sheria ya manunuzi ya umma (Public Procurement Law) ambayo inapelekea taifa kutumia pesa zu umma kuwaneemesha wauzaji na wakandarasi wa ndani na nje ambao siyo wazawa.

Katika muda wa miaka michache, sekta ya ujenzi nchini imechukuliwa kwa ujumla wake na wakandarasi kutoka China. Kabla ya hapo sekta hiyo iliendeshwa kwa kiasi kikubwa na wakandarasi kutoka Ulaya. Makampuni ya wazawa yenye uwezo kitaaluma yamebaki kuwa sub-contractors wa kudumu wa makampuni haya ya nje. CHADEMA haijakemea sera hizi
Hivi majuzi gesi asilia ilipogunduliwa nchini, Serikali iliyopo madarakani imeonyesha wazi kutokuwa na nia

ya kushirikisha wazawa katika sekta hii muhimu. Hatujaona CHADEMA ikitoa msimamo tofauti dhidi ya sera hii potofu.

CHADEMA ina wafuasi wengi vijana na wengi wao hawana kazi wala matumaini ya kupata kazi kama nchi itandelea kusimamia uchumi wake kwa sera zilizopo za business as usual (misaada, madeni na kodi za kulazimishana). Sera ya CHADEMA kuhusu ni vipi itasimamia uchumi kuleta matumaini kwa vijana na kwa kuishirikisha sekta binafsi haijulikani.

Kwa chama ambacho kimetamka rasmi imani yake katika uchumi huria na kuahidi kuimarisha sekta binafsi nchini, hatujaona chama kikiwa na mwamko wa kutaka kuwa na uhusiano wa karibu na sekta binafsi nchini hasa sekta binafsi ya wazawa. Au

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

niseme katika hili hakuna tofauti kati ya CHADEMA na CCM.

Kutokuwepo na msimamo unaoeleweka wazi kwa wote ndani na nje ya chama ambao ni tofauti na msimamo uliopo sasa kuhusu itikadi ya chama na hasa kuhusu usimamizi na uendeshaji wa uchumi ni kikwazo kikubwa kwa sekta binafsi.

Wadau wa uchumi katika sekta binafsi hasa wazawa wana wasiwasi mkubwa kuhusu mustakbali wa nchi katika siku na miaka ijayo kwani sera zinazotekelezwa hivi sasa zimeshindwa na hatufahamu kama kuna chama chenye fikra mpya kuhusu namna ya kuendesha uchumi wa nchi unaoshirikisha na kuwanufaisha wananchi wa Tanzania walio wengi.

Ingekuwa vema kama CHADEMA, chama kikuu cha upinzani nchini na chama chenye ushawishi mkubwa kwenye jamii na chenye uwezo wa kutawala nchi kwa ridhaa ya wananchi katika muda usio mrefu, kingetamka upya itikadi yake ya siasa na mwelekeo wa uchumi na kufuatisha kwa vitendo matamko hayo.

**Political Management of the National Economy**
**Presentation to the CHADEMA Leaders' Retreat**
**By: Ali A. Mufuruki. Chairman CEO Roundtable of Tanzania**
**Machame – Moshi. 9th January 2014**

Bila hivyo wananchi wataendelea kuchanganyikiwa kuhusu ni nani katika vyama vya siasa vilivyopo ataweza kuikomboa nchi yetu kutoka katika janga la umaskini na kuweka hatamu za kuendesha uchumi wa nchi hii mikononi mwa wananchi wake wazawa.

Ahsanteni